

**Mradi Na. 4234: Mfumo wa Anwani za Makazi:**

Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 **Sh. 40,000,000,000** fedha za ndani zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Mfumo wa Anwani za Makazi. Katika hotuba ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 vipaumbele vilivyoainishwa kwenye mradi huu ni:

- (i) Kuhakiki miundombinu iliyowekwa wakati wa Operesheni Anwani za Makazi ili kuhakikisha viwango vimezingatiwa ili Mfumo uwe na tija kwa wananchi na kuwa endelevu;
- (ii) Kuhakiki taarifa zilizokusanywa kwenye operesheni maalum ya utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi;
- (iii) Kuboresha Kanzidata na Programu Tumizi ya Mfumo;
- (iv) Kuendelea kuunganisha Mfumo wa Anwani za Makazi na Mifumo mingine ya kutoa huduma muhimu za kijamii;
- (v) Kutoa elimu kwa umma; makundi maalum ya kijamii kuhusu manufaa na matumizi sahihi ya Mfumo na kujengea uwezo Taasisi za umma na binafsi kutoa huduma kupitia Mfumo;
- (vi) Kutunga Sheria ndogo za kuwezesha ujenzi na matumizi ya Mfumo, mapitio ya Sheria ya EPOCA na Kanuni zake kuwezesha matumizi ya Mfumo;
- (vii) Kununua servers mbili (2) kwa ajili ya kuhifadhi taarifa za Mfumo na vifaa vya kuwezesha matumizi ya Mfumo;
- (viii) Kuandaa mwongozo wa kufanya maboresho ya namna mpya ya kufanya biashara kwa kutumia Mfumo;
- (ix) Kutengeneza Mkakati wa usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa Mfumo; na
- (x) Kuwezesha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mfumo.

Hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2022 Wizara ilipokea jumla ya kiasi cha Sh. 7,000,000,000 sawa na asilimia 17.5 ya bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Mradi tajwa. Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi husika ni kama ifuatavyo: -

- (i) Kufanya uhakiki wa taarifa za Anwani za Makazi kwenye Halmashauri 12, ambazo ni Majiji ya Dodoma, Arusha, Mbeya na Tanga, Manispaa za Mjini, Magharibi A, Magharibi B na Moshi; na Halmashauri za Kaskazini A, Kaskazini B, Kusini na Kati;
- (ii) Kuboresha Mfumo wa Kidijitali wa Anwani za Makazi;
- (iii) Kuandaa Mapendekezo ya maboresho ya sheria za kusimamia Anwani za Makazi;

- (iv) Kutoa elimu kwa Umma kuhusu Anwani za Makazi;
- (v) Kuandaa Muundo wa usimamizi na uendeshaji wa Mfumo wa Anuani za Makazi;
- (vi) Wizara imefanikiwa kutunga Kanuni ndogo za Anuani za Makazi ambazo zimetumika katika kutekeleza mradi wa Anwani ya Makazi.